

## Excerpts from the speech of Hon. Hawa Ghasia (MP), Minister for Regional Administration and Local Government

“Ninayo furaha kubwa leo hii kukutana nanyi nyote katika hafla hii ya ufunguzi wa Semina elekezi ya mpango wa Kuitafiti Elimu ujulikanao kama ‘**KiuFunza**’. Malengo ya mradi huu ni kupata ufumbuzi wa changamoto muhimu ambazo zinaikabili Nchi yetu katika kutoa elimu kwa watoto na vijana wetu.”

“Kama mjuavyo, elimu ndio msingi wa maendeleo ya jamii yoyote ile. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere baada ya Tanganyika kupata uhuru aliiona elimu kama chombo cha kuikomboa nchi na Bara la Afrika kwa ujumla. Leo hii, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete pia anatambua ukweli huo na kwa sababu hiyo amekua mstari wa mbele katika kupanua fursa za elimu kwa ngazi zote.”

“Hivyo, Elimu ndio injini madhubuti ya kuifikisha jamii kwenye kilele cha maendeleo.”

“Hivyo basi, changamoto tulizonazo hivi sasa sio wingi wa wanafunzi walio shuleni bali kutoa **Elimu Bora kwa Wote**, yaani watoto na vijana wote walioko shuleni. Mafanikio tuliyopata katika kupanua fursa za elimu yata potea endapo wanaohitimu katika ngazi yoyote watakuwa hawana stadi na maarifa wanayohitaji kwa ajili ya maisha yao, ajira au kujijiri. Kwa hiyo tunalazimika hivi sasa kutafuta mbinu na taratibu za kiutendaji ambazo zitachochea kujifunza na kupata elimu iliyo kamilifu.”

“Semina hii ni muhimu kwa kuwa lengo lake ni kutafiti ili zipatikane mbinu na taratibu za kiutendaji zitakazoleta ufanisi katika kufundisha na kujifunza.”

“Lengo kuu chini ya mpango huu wa ‘**KiuFunza**’ ni kwamba; tufanye nini ili watoto waweze kukuza stadi za kusoma na kuhesabu katika darasa la Kwanza hadi la Tatu; kwani huu ndio msingi madhubuti wa elimu kwa kuwa ni kweli mtoto hawezi kukimbia kabla ya kutambaa; wala nyumba haiwezi kuzekwa kabla msingi haujajengwa.”

“Jambo kuu katika utafiti utakaofanywa chini ya mpango huu wa ‘**KiuFunza**’ ni kupata njia mbadala kwa kutumia mawazo mawili makuu. Kwanza ni kutafiti juu ya taratibu muafaka za kutoa kiwango cha fedha za uendeshaji wa shule ya msingi “CG” kwa muda unaotakiwa na kwa uwazi zaidi na pili; jinsi ya kuwamotisha walimu pale ufundishaji wao unapowezesha watoto kujifunza kwa ufanisi kuliko ilivyo sasa – yaani ‘cash on delivery’.”

“Napenda kueleza kuwa wazo hili la motisha au bahshishi ni jipya hapa nchini, yaani – kumpa mwalimu bahshishi kulingana na matokeo ya kazi ya kufundisha. Nieleze hapa kwamba, wazo hili limetokana na mawazo ambayo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyapata alipoitembelea Taasisi ya Maendeleo ya “*Center for Global Development*” huko Marekani.”

“Suala la kuwa wabunifu ni lina umuhimu wa kipekee katika mambo ya elimu. Watendaji katika Sekta hii lazima wawe tayari kupokea mawazo mapya. Hatuwezi kuongeza ubora wa elimu kwa kutegemea au kutumia taratibu na mbinu zililizile ambazo zimetumika kwa miaka 40 iliyopita la hashu, Dunia sasa imebadilika, zimezuka changamoto mpya, na zipo pia fursa mpya. Upo ushahidi wa kisayansi kuhusu mbinu ambazo zimeleta mafanikio mahali pengine Duniani; Je hizi zinaweza kutumika hapa Tanzania.”

“Katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo makubwa kama haya ya kielimu, lazima pia tuangalie thamani ya uwekezaji wetu. Je, uwekezaji huo umekuwa na matokeo gani? Ninatumaini kuwa tafiti

zitakazofanywa zitatoa ushahidi kuhusu mambo ambayo yataleta ubora katika elimu ili uamuzi wa kiseru na kiutendaji uwe na tija na uwe wa nafuu kifedha.”

“Mwisho, kama inavyotegemewa Serikali iko tayari kupokea mawazo mapya yatokanayo na ushahidi wa kisayansi. Hivyo, ninaamini utekelezaji wa mradi huu utakuwa wa wazi pia. Fanyeni mawasiliano na Mikoa, Halmashauri na Shule zitakazochaguliwa kwa uwazi na pia kutoa taarifa za jinsi kazi inavyoendelea. Ninaamini pia kuwa mtafanya majumuisho ya matokeo ya utafiti huu kwa uwazi pia ili watunga sera waweze kutumia matokeo hayo kuandaa sera na mipango itakayokuwa na tija kielimu.”